


**CHANGAMOTO ZA KISARUFI MIONGONI MWA WANAFUNZI WA KISWAHILI
WA SHULE ZA UPILI WILAYANI KATHONZWENI JIMBO LA MAKUENI.**

**RIPOTI HII IMEWASILISHA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA
KATIKA CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

JINA: MARGARET MWONGELI KITIVI

NAMBARI: BEDA – 24348 / 2013



MURIITHI J. J.

IKISIRI

Ripoti hii ya utafiti lilitarajia kuchunguza 'changamoto za kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Kathonzweni jimbo la Makueni'. Katika utafiti huu, makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi hawa ndiyo yaliyochunguzwa kwani kipengele hiki kilichukuliwa kama kiini cha lugha yeyote ile. Vipengele vingine vya sarufi viliingiliana nacho na kukitegemea kwa kiwango kikubwa. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kubainisha makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Kathonzweni, kuainisha makosa hayo; kuyaeleza na kutathmini mikakati iliyozingatiwa kupunguza makosa hayo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi makosa (um) na ile ya lugha kadirifu (lk). UM ulitilia mkazo mbinu ya kuchunguza lugha ya mwanafunzi kwa kubainisha makosa aliyoyafanya, aina za makosa hayo, kuyaeleza na kuyatathmini. Nayo LK ilichunguza lugha ya mwanafunzi kwa kuzingatia mikakati ya kisaikolojia katika mchakato ulioendelea wa ujifunzaji wa L2. Katika LK, vyanzo vya makosa yaliyofanywa na mwanafunzi vilichunguzwa kutegemea mikakati hiyo ya kisaikolojia ambayo mwanafunzi alitumia katika jitihada zake za kujifunza L2. Kwa hivyo kupitia uzingatifu wa nadharia hizi, matokeo ya utafiti huu yalisaidia. Kutoa mapendekezo mwafaka kwa washikadau wa ufundishaji wa Kiswahili wa shule za upili nchini Kenya ili kupunguza makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi hawa. Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo na data zilikusanywa nyanjani kwa kuzihusisha shule tatu za upili wilayani Kathonzweni ambazo ni kitise, Kiangini and Mbuvo. Mbinu ya kimakusudi ilizingatiwa katika usampulishaji na watafiti walipatikana kwa kutumia mbinu nasibu ambapo wanafunzi kumi walichaguliwa katika madarasa ya pili and nne kutoka kila shule iliyoteuliwa. Hojaji na mahojiano ndiyo yaliyozingatia na mtafiti kukusanya data kutoka kwa wanafunzi hao na walimu wao. Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa njia ya kimaelezo ambapo majedwali na vielelezo vilitumika ili kufafanua zaidi matokeo ya utafiti.